

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA



TANGAZO KWA MAWAKILI WOTE

YAH: UHUISHAJI WA LESENI ZA UWAKILI KWA MWAKA 2019

Tangazo hili limetolewa leo siku ya Alhamisi tarehe 20 Desemba, 2018.

Mawakili wote mnajulishwa kwamba zoezi la kuhuisha Leseni za Uwakili kwa ajili ya Mwaka 2019 lilianza rasmi tarehe 10 Desemba, 2018 kupitia mfumo wa **Tanzania Advocates Management System (TAMS)**. Hivyo, Mawakili wote mnasisitizwa kuhuisha Leseni zenu mapema kabla au ifikapo tarehe **31 Januari, 2019** ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na kulipa faini ya kuchelewa kuhuisha na pia ni kosa kufanya kazi ya uwakili bila kuwa na Leseni iliyo hai.

Aidha, mnajulishwa kwamba Namba za Kumbukumbu ya malipo **“Control Number”** kwa ajili ya ada za Mahakama zinapatikana kwenye mfumo wa TAMS kupitia akaunti zenu. Kwa mantiki hiyo, mnasisitizwa kulipa kwa kutumia namba za kumbukumbu mtakazopewa na mfumo kupitia akaunti zenu binafsi katika TAMS baada ya kukamilisha vigezo ili kurahisisha zoezi la Uhuishaji wa Leseni za Uwakili.

Vilevile, mnafahamishwa kwamba mtalazimika kujaza taarifa zote muhimu kwenye akaunti zenu za TAMS ikiwa ni pamoja na kuhakikisha umekidhi vigezo na matakwa ya kupewa Leseni ili kuweza kupata Leseni za Uwakili kwa Mwaka 2019 kama mfumo utakavyokuongoza. Aidha, mnahimizwa kurejea mwongozo uliopo kwenye mfumo wa TAMS kwa maelekezo zaidi .

Kwa Mawakili ambao wamelipia ada za Mahakama nje ya mfumo wa TAMS, wanaelekezwa kuvuta subira hadi mapema Januari, 2019 ambapo suala lao litashughulikiwa.

Iwapo Wakili atakuwa na swali au atakutana na changamoto yoyote tafadhali asisite kuwasiliana na Ofisi ya Msajili wa Mahakama Kuu (T) kwa anuani ya barua pepe rhc@judiciary.go.tz

Nawatakieni utekelezaji mwema.

**IMETOLEWA NA OFISI YA MSAJILI
MAHAKAMA KUU (T)**